
# MIMI NI NANI?



MAFUNDISHO YA BIBLIA KWA VIJANA WA KIAFRIKA

## MWALIMU

ni zawadi ya Mungu. Lakini tunaokolewa ili tuyatende matendo mema, yaani kwa kutumia wengine.

"Katika kuyatimiza mapenzi ya Baba, kuna mambo mawili yaliyo na lazima. Ni lazima tuyafahamu mapenzi yake na tuyatimize. Hekima na utii ni maneno yaliyo muhimu katika Agano Jipya. Kama tunataka kuwa wanafunzi wa Yesu ni lazima tuanze kwa msingi imara wa kuyajua mapenzi ya Mungu na kuyafanya. Mpango wake ni kuwa wewe uwe mkamilifu kama yeye alivyomkamilifu. Unaweza tu kuuelekeza mpango huo kwa kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu kwa njia ya maombi, masomo ya Biblia na kwa kumfuata yeye."

Wanafunzi warudie Kifungu cha Kukumbuka mpaka waweze kukisema bila msaada. Wakumbushe Kazi ya Kufanya katika vitabu vyao.

**Maombi**

1. Mwombee kila mwanafunzi akue na kukomaa katika imani yake ya Kikristo.

2. Omba kuwa kila mmoja atakuwa na ari ya kuwa mwanafunzi wa Kristo bila kufikiria gharama.

3. Mwombe Mungu akuongoze ili uwe mkamilifu kadiri utembeavyo karibu naye.



# MIMI NI NANI?

## KITABU CHA MWALIMU

## MAFUNDISHO YA BIBLIA KWA VIJANA WA KIAFRIKA

Africa Coordinated Curriculum
for Bible Study

Y2 - 1Ts

Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI

© Copyright, 1986
Baptist Publications House
All rights reserved



tumekwisha okolewa. Hatuifanyi ili tuweze kuokolewa. Wajibu wetu katika wokovu ni kupokea tu zawadi ya Mungu. Sisi wenyewe tukishaokolewa basi tutamtaka yeye atutumie sisi ili tuwasaidie watu wengine waokolewe. Soma Wafilipi 2:15 tena.

**Maelezo**

Sema: "Tunakuwa wana wa Mungu tunapompokea Kristo katika maisha yetu na kuliamini jina lake. Mungu anao mpango na kila mwana wake. Wajibu wetu ni kuuelewa mpango huo na kuutekeleza. Mkristo aliyefanikiwa ni yule ayafanyaye mapenzi ya Mungu. Katika sura ya saba tumekwisha eleza jinsi ya kufahamu mapenzi ya Mungu katika maisha yetu. Tatizo letu sasa ni kuupata mpango wa Mungu kwa maisha yetu.

"Katika Wafilipi 2:12-15 tunaelezwa kuwa ni mapenzi ya Mungu kwa wana wake kuwa watakuwa wasio na hatia, waaminifu, wana wa Mungu wasio na waa. Je, haya twawezaje kuyapata? Tutawezaje kuwa wakamilifu? Hamwezi kupata jibu lake katika habari hii lakini labda unaweza ukakumbuka kutokana na mafundisho tuliyokwisha soma hapo mbeleni. Kama hukumbuki basi angalia kwa haraka katika sehemu ya Mafunzo ya Sura Hii Kwangu, sura ya kwanza na ya pili kuona kama hayo yatakukumbusha. Je, tutawezaje kuwa watimilifu kama Baba yetu wa mbinguni alivyomtimilifu?

**Ukweli Katika Maisha Yangu**

Sema, "Huu ni wakati wa matendo. Bwana Yesu anahitaji wanafunzi leo. Anawahitaji wale ambao wamejitenga na dhambi na ubinafsi. Anawataka wale watu ambao wako tayari kufanya mapenzi yake. Anawataka wale watu ambao wako tayari kuwa watumishi. Anawahitaji wana wasio na hatia wala waa. Hatuokolewi kwa ajili ya matendo yetu mema. Wokovu

Kristo kama sisi tulivyo leo. Yeye ndiye Bwana ambaye wote wahitajiwa wampe utukufu, ambaye vyote ni vyake. Utukufu kwa wanadamu ndicho chanzo cha migawanyiko katika makanisa yetu hata leo.

Kwa njia ya sala za Paulo Wakristo wa Kolosai walijazwa kwa uwezo wa mapenzi ya Mungu katika hekima yote na uwezo wa kiroho wote (Kolosai 1:9). Kusudi la hayo yote ni dhahiri, ili waweze kutembea katika wito wa Bwana. Huko Kolosai Wakristo walifundishwa mafundisho ya uongo. Kwa sababu ya kuuhatarisha ukweli ndiyo sababu tunamwona Paulo akiwaombea kama ilivyo andikwa katika Wakolosai 1:9-10. Kuyafanya mapenzi ya Mungu ndicho kitu muhimu sana katika maisha ya Mkristo. Je, utayafahamu kwa jinsi gani hayo mapenzi?

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Sema: "Ni mapenzi ya Mungu kuwa watu wote waokolewe na kupata kujua yaliyo kweli." Mmoja some I Timotheo 2:3-4.

Sema: "Waefeso 2:8-9 inatueleza jinsi ya kuokolewa. Wokovu ni zawadi ya Mungu. Tunaokolewa kwa neema ya Mungu.

"Je unafanya nini na vile vitu unavyopewa? Ikubali hiyo zawadi na kuitumia.

"Mmoja wenu asome Wafilipi 2:12-15. Je, maneno, '...utimizeni wokovu wenu...' yana maana gani kwako? Je, unafikiri kifungu hiki kinatofautiana na Waefeso 2:8-9? Je, tunaokolewa kwa neema au kwa yale tunayofanya?

"Tunaokolewa kwa neema ambayo ni kipawa cha Mungu kwetu. Hatuwezi kutumika ili tuupate wokovu. Kazi yo yote tufanyayo kwa ufalme wa Mungu ni kwa sababu tayari



## YALIYOMO


SURA — UKURASA

1. Kuumbwa Kwangu .......... 5
2. Kuzaliwa Kwangu .......... 10
3. Mwili Wangu .......... 14
4. Dunia Yangu .......... 19
5. Muda Wangu: Wake au Wangu .......... 23
6. Maumbile Yangu: Yake au Yangu .......... 28
7. Mapenzi Yangu: Yake au Yangu .......... 33
8. Mwenendo Mzuri .......... 37
9. Unajenga Nini? .......... 42
10. Wewe U Mtumishi? .......... 46
11. Mnahusianaje? .......... 51
12. Je, Uko Tayari Kuongoza? .......... 56
13. Vyote ni Vya Mungu .......... 61

## KUHUSU MWANDISHI

Mwandishi wa kitabu hiki ni Moses M. Ochwo. Alizaliwa katika Uganda, na amefundisha katika Shule za Sekondari kwa muda wa miaka 13 hali akiwa pia Mkuu wa Idara ya Elimu ya Kikristo.

Ochwo ameoa, na anayo Diploma ya Elimu kutoka Chuo Kikuu cha Makerere. Sasa yeye ni Katibu na Mkurugenzi wa Injili na Huduma za Enezi katika Umoja wa Makanisa ya Kibatisti ya Uganda.

SURA YA KUMI NA TATU

# VYOTE NI VYA MUNGU

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: 1 Wakorintho 3:21-23; Wakolosai 1:9-10

Vifungu vya Leo: Wafilipi 2:12-15

**Kifungu cha Kukumbuka:**

> "Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni" (Mathayo 7:21).

Kusudi la Somo Hili: Kuwasaidia wanafunzi wayatafute mapenzi ya Mungu na wajue jinsi ya kuyapata.

Vitu Vya Kusaidia Kufundisha: Ubao au karatasi kubwa. Andika hicho kichwa ubaoni.

**Msingi wa Somo Hili**

Waraka wa kwanza wa Wakorintho 3:21-23 unatuonya kuwa tusiwape wanadamu utukufu. Kanisa la kule Korintho liligawanyika kwa sababu ya viongozi fulani waliokwenda huko Korintho kutoa huduma. Kwa vyo vyote, kulikuweko na tofauti kati ya wahudumu hao, lakini tofauti hizo lengo lake lilikuwa si kuleta utengano. Kazi ya tofauti hizo ilikuwa ni kukamilisha utumishi wa kila mmoja. Wakristo wa Korintho hawakuelewa hilo. Badala yake walijigawa katika makundi yanayopingana. Kila kikundi kilijiona kina ukweli, na hekima na kujivunia kiongozi wao waliyempenda.

Lakini viongozi hawa walikuwa ni watumishi tu na kila mmoja alikuwa sehemu nzima ya kanisa. Kwa kuviruhusu vikundi kama hivyo viendelee, Wakristo wa Korintho walionyesha kuwa hawaelewi ya kuwa wao wote walikuwa wa

2. Mwombee kila mmoja awe na ari ya kutumika na kunyenyekea.

3. Omba kuwa wewe utawaonyesha mfano mzuri wa utumishi na unyenyekevu.



SURA YA KWANZA

# KUUMBWA KWANGU

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Zaburi 8; Wakolosai 1:16-17

Vifungu vya Leo: Zaburi 8:3-6; Matendo 17:28

**Kifungu cha Kukumbuka:**

> "Jueni kwamba Bwana ndiye Mungu; Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake; Tu watu wake, na kondoo wa malisho yake" (Zaburi 100:3).

Kusudi la Somo Hili: Ni kuwasaidia wanafunzi watambue kuwa Mungu aliwaumba kwa mfano wake na kwa utukufu wake na kwa ushirika naye.

Vitu Vya Kusaidia Kufundisha: Ubao au karatasi kubwa ya kuandika kichwa cha somo. Pia utahitaji kitambaa cha kufunga macho ya mmojawapo.

**Msingi wa Somo Hili**

Mambo muhimu katika Zaburi 8, ni kuwepo kwa Mungu na kazi zake hapa duniani. Tunaweza kuona ukuu wa jina lake (kifungu cha 1) katika kazi yake duniani. Watoto wachanga waimbe na kumsifu, na utukufu wake ufike hata mbinguni. Anao ushindi juu ya adui zake (vifungu 1-2).

Vifungu 3-8 vinaeleza jinsi ilivyo vigumu kuelewa njia za Mungu - hasa jinsi anavyomchukulia mwanadamu. Kulinganisha na viumbe wengine, mwanadamu ni mdogo sana. Pamoja na hayo, Mungu anamfanyia tofauti na viumbe wengine. Mungu anamfikiria na kumtunza. Mwandishi wa Zaburi anaendelea kwa kueleza mambo yanayomfanya mwanadamu kuwa tofauti na viumbe wengine.

*Anafanywa mdogo punde kuliko Mungu.* Ni mdogo kwa maana mwili wake unaoza sawa na viumbe wengine. Lakini uhai wake ni wa kiroho, usio kufa na una ubora wa kumfanya kiumbe wa mbinguni. Ni yeye pekee aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu.

*Mungu amemvisha taji ya utukufu na heshima.* Mungu amempa busara kuliko wanyama wa nchi na ndege wa angani. Lakini ana mambo mengine zaidi kama haki, kujitawala, akili na kuthaminika. Mambo hayo bora yamemfanya mwanadamu kuwa kiumbe wa hali ya juu kuliko viumbe wengine.

*Amemfanya mtawala juu ya kazi ya mikono yake.* Mungu ameweka dunia na vyote vilivyomo chini ya utawala wa mwanadamu. Mungu amempa pia uwezo wa kuvitawala.

Katika Wakolosai 1:16-17, tunapewa habari zaidi jinsi ulimwengu ulivyoumbwa na uhusiano wake na Yesu Kristo. Yesu ni chanzo, lengo na umoja wa uumbaji. Vitu vyote viliumbwa kwa njia yake. Vitu vyote viliumbwa kwa ajili yake. Vitu vyote vimeshikana katika yeye. Mwanadamu ameumbwa kwa ajili ya Kristo. Tumewekwa pamoja katika umoja wa Kristo.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Sema: "Somo la leo ni juu yetu wenyewe. Sisi ni nani? Wewe ni nani? Nataka kuanza kwa kuwaeleza hadithi fupi.

"Kulikuwa na mwanafunzi mmoja aliyekuwa ana tatizwa kila asubuhi. Alikuwa hawezi kukumbuka alipokuwa ameweka vitu vyake usiku uliotangulia.

"Siku moja aliamua kutatua tatizo lake. Aliamua kuandika kila kitu kitabuni nà mahali ambapo huweka kabla ya kwenda kulala. Usiku ule aliandika kwenye kitabu chake hivi:- 'Koti





2. *Kiongozi ni mtu anayenyenyekea.* Yeye yuko tayari hata kufanya kazi zile zilizo chafu (kama kuosha miguu) kama hilo litawasaidia watu wake. Yeye hana majivuno wala hatafuti mambo kwa ajili yake mwenyewe.

"Kumbuka kuwa huo sio mtazamo wa dunia wa kiongozi. Dunia inamwangalia kiongozi kama yule anayetumikiwa na siyo kama yule anayetumika."

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema, "Kutokana na hilo somo tunaona yakuwa *kila Mkristo ameitwa ili aongoze,* kwa sababu kila Mkristo ameitwa ili atumike. Hii maana yake si kuwa kila Mkristo ameitwa kuwa Bwana Mtawala. Bwana mtawala ni mtu yule aliye na kipawa cha kuongoza wengine. Lakini Mkristo anaweza kuwaongoza wengine kwa kuwaonyesha mifano bora, hasa mfano wa utumishi. Dunia hii haihitaji mabwana. Inahitaji watumishi. Kila Mkristo anaweza kutumika na tumepewa zawadi ili tusaidie katika utumishi huu. Je, wewe uko tayari kuongoza?

"Kila kiongozi lazima anyenyekee. Kunyenyekea maana yake sio tu kuzifanya kazi zile zilizo chafu. Hii ni pamoja na kufundishika, kujiweka tayari kuwasikiliza wengine. Yesu aliwachagua wale mitume kumi na wawili kama viongozi wa kanisa. Katika Yohana 13 alikuwa akiwafundisha na kuwaongoza. Wao walipaswa kusikiliza na kuwa tayari kujifunza."

Wanafunzi warudie Kifungu cha Kukumbuka. Wakumbushe juu ya Kazi ya Kufanya katika vitabu vyao.

**Kuomba**

1. Omba kuwa wanafunzi wataelewa maana ya uongozi wa kweli ni nini.

"Tafadhali mmoja wenu asome kwa sauti sehemu ya Utangulizi katika vitabu vyenu. Unafikiri kwa nini kuna watu wanaopenda kuwaongoza wengine? Wanategemea kupata nini kutokana na hilo? Waweje? Je, ungependa uwe kiongozi? Kwa nini unayo ari hiyo?

"Tuseme shule yako au kijiji chako kinafuata utaratibu wakidemokrasia wa kuwachagua viongozi, viranja au machifu. Jifanye kama mmoja wa wale wanaopenda wachaguliwe. Je, ili watu wapate ukuchagua, katika hotuba yako ungesema nini? Andika orodha ya mambo haya katika karatasi yako wakati darasa lote linatoa majibu yao" Waruhusu wanafunzi watoe sababu kwa nini wangechaguliwa.

"Sasa hebu tusome Yohana 13:12-17. Nani anapenda kusoma vifungu hivi?" (Wape muda wa kusoma.)

Uliza, "Je, ni mafundisho gani mawili muhimu ambayo Yesu alikuwa anawafundisha wanafunzi wake? Je, kuna uhusiano gani kati ya mafundisho haya na ile orodha uliyoandika dakika chache zilizopita?"

**Maelezo**

Sema: "Mafundisho haya mawili ni:

1. *Kiongozi ni mtumishi.* Yesu alikuwa kiongozi. Lakini bado aliosha miguu ya wanafunzi wake. Tunapofikiria kuhusu uongozi, wengi wetu kufikiria kuhusu madaraka, heshima na mapendeleo yatokanayo na uongozi huo. Je, huwa tunawafikiria wale tunao waongoza? Je, mahitaji yao na matatizo yao ni yapi? Tutaweza kufanya nini ili tuweze kuwasaidia?

"Yesu ndiye mchungaji mwema anawaelewa watu wake: majina yao; mahitaji yao, na matatizo yao. Yeye huwaita na kuwaongoza kwenda kule mahitahi yao yaliko (Yohana 10:3).





langu liko juu ya meza, viatu chini ya kitanda, nami niko juu ya kitanda.'

"Siku ya pili aliweza kupata vitu vyote isipokuwa yeye mwenyewe. Hakuwa juu ya kitanda. 'Niko wapi?' alianza kuuliza. Alianza kulia. Hakuweza kujikuta. Je, unafikiri hii ni hadithi ya kijinga au ni tatizo kwa watu wengi? Watu wengi hawajijui wao ni nani au wako wapi.

"Sasa nataka mmoja wenu aje hapa mbele ili nimfunge kitambaa machoni. Nataka mwingine aje mbele ya huyu asiyeweza kuona sasa na tuone kama ataweza kumtambua kwa sauti. Utasema tu 'Mimi ni nani?'" Baada ya huu mchezo mfupi uliza, "Unafikiri swali lako lilijibiwa vizuri hata ukaridhika? Je, wewe ni jina peke yake? Soma Zaburi 8:3-6. Unajifunza nini juu ya mwanadamu katika vifungu hivi?" (Mwambie mmoja asome.)

**Maelezo**

Sema, "Tunaweza kuona majibu mengi sana kwa swali hilo. Mimi ni nani? Mmoja anaweza kusema, "Mimi ni Thomas. Ni mwana wa wazazi fulani. Mimi ni wa taifa na kabila fulani. Mimi ni mwanafunzi wa shule ya sekondari.

"Je, ni mambo gani unayoweza kueleza juu ya mtu, kwa mtu asiyemfahamu?" Kwa mambo yaliyotajwa majibu yanaweza kuwa; elimu, desturi za maisha, siasa, uwezo wa kufikiri, maumbile, mapendeleo na dini.

Sema, "Zaburi uliyosoma sasa hivi inatupa mambo ya kweli muhimu matatu juu ya mwanadamu. Kwanza inatuambia kuwa mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Alimuumba mdogo punde kuliko Mungu mwenyewe. Maana ya mfano huu unaelezwa katika kitabu chako. Funua sehemu ya maelezo na kusoma juu ya mfano." Ruhusu kama dakika tatu kwa kusoma.

Sema: "Mwanadamu ana mfano wa Mungu ndani yake, lakini ule mfano umeharibiwa na dhambi. Tunaambiwa pia kuwa mwanadamu alivishwa taji ya utukufu na heshima. Utukufu na heshima vinaonyesha ule ubora unaomfanya mwanadamu kuwa tofauti na wanyama wengine. Unafikiri ni tofauti zipi zilizopo kati yako na wanyama?" Ngojea majibu. "Mungu amempa mwanadamu mamlaka juu ya viumbe vingine vyote. Unafikiri mwanadamu bado anazo nguvu juu ya viumbe vingine?"

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Angalia sehemu ya mafunzo katika sura hii kwenye kitabu chako.

1. Ni nini kinachonifanya niwe tofauti na wanyama?
2. Kwa nini Mungu aliniumba kwa mfano wake?
3. Mungu anafanya nini kuhifadhi ule mfano wa Mungu ndani yangu?
4. Nitafanya nini kumruhusu Roho Mtakatifu ahifadhi mfano wa Mungu ndani yangu?

"Mungu alimuumba mwanadamu kwa mfano wake kwa sababu ya uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu. Uhusiano huo uliharibiwa na dhambi lakini kwa njia ya Kristo unaweza kurudishwa. Tunaweza kumpenda Mungu kwa moyo wetu wote kwa akili zetu zote, na kwa roho zetu zote na kupenda jirani zetu kama tunavyojipenda wenyewe."

Wasaidie wanafunzi kujifunza Kifungu cha Kukumbuka. Wakumbushe juu ya Kazi ya Kufanya.

**Kuomba**

1. Omba kuwa wanafunzi wataona kuwa wanao wito mkuu. Wito huu unahusiana kati yao na Mungu na watu wengine.





Je, wajibu wa mwanadamu kwa Mungu wa jinsi hiyo uwe ni nini? Daudi anatueleza katika Zaburi hii kuwa matumaini yake yote ni katika Bwana, kama kondoo anavyomtumaini mchungaji. Mtu anapoyaelewa mapenzi ya Mungu, anaburudika akilini mwake na kuwa huru. Hakuna wasiwasi kwa yule anayetegemea mapenzi ya Mungu. Wakati mwingine safari hiyo ni ya matatizo, na tumezungukwa na adui wengi, lakini jambo hili halitaweza kumwondolea matumaini yule aliyeiweka imani yake katika Mungu.

Wakati Daudi alipoangalia picha ya Mungu kama mwenyeji, anasema kuwa Mungu ni mwenyeji aliyetimilika. Mwenyeji hutoa chakula na kuwafurahisha na kuwalinda wageni wake wasidhuriwe na adui. Uhusiano wa baraka na Mungu hauna kikomo. Bwana ni kiongozi anayetumikia.

Katika Mathayo 28:18-20, tunasoma juu ya uongozi wa Kristo, madaraka yote mbinguni na duniani amepewa yeye. Ameahidi kuwaongoza watu wake po pote waendapo, na kuwa nao nyakati zote. Hata kama tu dhaifu kiasi gani au hata kama yale tuyafanyayo si muhimu, Yesu ni rafiki na mwenzetu. Hatuwezi kumuona kwa macho yetu, lakini yeye yupo kutulinda kutuongoza na kutuhifadhi. Yeye ndiye mchungaji mwema.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Sema, "Leo tutajifunza kuhusu uongozi na hasa uongozi kama vile unavyofundishwa katika Biblia.

"Viongozi wapo katika jamii zote katika jamaa, katika viwanda, katika mashule, katika nchi na katika makanisa. Inakuwa kama hakuna jamii itakayoweza kuishi bila viongozi. Wajibu wetu leo ni kutafuta nini maana ya uongozi kutokana na msimamo wa Biblia.

SURA YA KUMI NA MBILI

# JE UKO TAYARI KUONGOZA?

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Zaburi 23, Mathayo 28:18-20

Vifungu vya Leo: Yohana 13:12-17; 10:3

**Kifungu cha Kukumbuka:**

> "Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe" (Matendo 20:28).

Kusudi la Somo Hili: Kuwasaidia wanafunzi waelewe maana ya uongozi wa Kikristo.

Vitu Vya Kusaidia Kufundisha: Karatasi na kalamu kwa kila mwanafunzi, ubao au karatasi kubwa. Andika kichwa hapo.

**Msingi wa Somo Hili**

Zaburi 23 inatueleza kuhusu uongozi wa Mungu na jinsi anavyotulinda katika mabadiliko mbali mbali ya maisha. Mungu amelinganishwa na mchungaji ambaye anaelewa kuwapa wanyama wake chakula, kuwalinda na kuwatosheleza. Zaburi hii inaeleza mambo tofauti yafanyikayo maishani mwa mwanadamu: akiwa ndani ya nyumba (kifungu cha 5-6), au nje (kifungu cha 1-2), ulinzi wa Roho kutokana na maovu (kifungu cha 3-4). Wakati wa majaribu (kifungu cha 4), wakati wa furaha (kifungu cha 5-6), ulinzi katika maisha (kifungu cha 6). Katika Zaburi hii hii, Mungu analinganisha na mwenyeji, nasi tu wageni wake. Mungu hutoa chakula kwa wageni wake.





2. Omba kuwa watapenda kuishi maisha yanayolingana na asili ya kuumbwa kwao.
3. Omba kuwa watayaona maisha hayo kwako.

SURA YA PILI

# KUZALIWA KWANGU

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Yohana 1:11-13; Mathayo 18:1-4

Vifungu vya Leo: Yohana 3:1-6; 1 Petro 2:2

**Kifungu cha Kukumbuka:**

> "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! yamekuwa mapya" (2 Wakorintho 5:17).

Kusudi la Somo Hili: Kuwasaidia wanafunzi wajifunze juu ya kuzaliwa kiroho na kukua Kikristo.

Vitu Vya Kusaidia Kufundisha: Karatasi na kalamu kwa kila mwanafunzi, ubao au karatasi kubwa.

**Msingi wa Somo Hili**

Kiini cha mahubiri ya Yesu kilikuwa ni ufalme wa Mungu (au wa mbinguni). Alifundisha mafundisho mengi kuhusu ufalme huu. Katika Mathayo 18:1-4, anafundisha jinsi mtu awezavyo kuingia katika ufalme yaani ni kubadilishwa na kubadilika jinsi unavyoishi. "...Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni" (kifungu cha 3). Tunapaswa kuwa kama mtoto mdogo.

Mtoto kwa asili ni mtiifu. Wakati mwingine hatii, wakati mwingine analalamika, lakini silika ya watoto ni kutii. Kama unahitaji maji ya kunywa, humtuma mtoto akuletee. Unaogopa kumtuma mtu mzima kwa sababu hujui majibu yake yatakuwa vipi. Ufalme wa Mungu umejengwa na watu wanao mtii Mungu. Kama unataka kuingia katika ufalme huo, ni lazima uwe tayari kutii pia.





2. Omba kuwa wewe na wanafunzi wako mtafuata mfano wa Yesu wa kutumika.
3. Omba ili juma hili uweze kupata nafasi ya kutumika.

1. *Kutubu:* Kutubu maana yake ni kuyaacha yale ambayo ya ubinafsi na dhambi na kumgeukia Mungu. Ubinafsi au kujipenda ndicho chanzo cha dhambi. Ndiye adui mkubwa wa binadamu.

"Mwanadamu alipoanguka na kuamua ajitegemee mwenyewe badala ya Mungu ambaye ndiye kiini cha maisha yake, matokeo yake yalikuwa sio tu mwanadamu ametengwa na Mungu. Bali uhusiano kati ya mwanadamu na mwanadamu mwenzake ulitoweka. Habari za ugomvi wa kwanza wa mwanadamu na Mungu katika sura ya 3 ya kitabu cha Mwanzo ina husiana na ile ya sura ya 4 juu ya ugomvi wa mwanadamu na mwanadamu. Kaini alimuua kaka yake Habili.

"Kama mwataka kuyafuata yale nifanyayo kuliko yale yaliyo ya Mungu, ni wazi kuwa nitataka kuyafuata mambo yangu mwenyewe kuliko ya watu wengine. Mtu hawezi kuonyesha uhuru wa mambo yake mwenyewe pasipo Mungu ili ajitoe kwa mtu mwingine. Lakini katika dunia ambayo kila mtu anataka kufanya mambo yake mwenyewe hawezi kuacha kuwa dunia iliyojaa wasiwasi, vizuizi, kutokuaminiana, kutokuelewana, magomvi na migongano.

2. *Uvae upendo.* Hali ya upendo wa jinsi hii umeelezwa kwa wazi katika 1 Wakorintho 13:4-8 na Wagalatia 5:22. Tafadhali soma vifungu hivi utakapo kwenda nyumbani leo.

Wanafunzi warudie Kifungu cha Kukumbuka. Wakumbushe Kazi ya Kufanya katika sehemu ya vitabu vyao.

**Kuomba**

1. Omba kuwa unaweza kuwasaidia wanafunzi waelewe kuwa tamaa ni nzuri lakini tamaa yao kubwa iwe ni kuwatumikia wengine na kumtumikia Mungu.





Mtoto anayo silika ya kusamehe. Watoto hugombana wenyewe kwa wenyewe, lakini baada ya muda mfupi wanakuwa marafiki tena. Ili tuweze kuingia katika ufalme wa Mungu, tunapaswa kusamehewa dhambi zetu. Hii ndiyo sababu ya Yesu kufa msalabani. Naye.alisema, "Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu" (Mathayo 6:14-15).

Kubadilishwa pia maana yake ni kuwa na uhusiano maalum na Mungu kama wana wake. Tunapompokea Kristo katika maisha yetu, tunafanywa watu wapya. Tumezaliwa mara ya pili (Yohana 1:11-13). Pasipo mabadiliko haya, hatuwezi kuingia katika ufalme wa Mungu (Yohana 3:1-6). Tunapompokea Kristo huja na kukaa ndani yetu kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Sema, "Somo hili hasa ni juu ya kuzaliwa mara ya pili. Wengi wetu hapa tutasema maana ya kuzaliwa mara ya pili.

Kwa kuanza tutajigawa katika makudi madogo madogo, kila kikundi kitakuwa na kazi ya kufanya. Unatakiwa umwandikie rafiki yako barua ambaye ameuliza swali, 'Kuzaliwa mara ya pili kuna maana gani?' Tutaisoma hiyo barua baada ya kumaliza kuiandika. Katika barua yako weka mawazo yafuatayao; Ina maana gani kuzaliwa mara ya pili? Kuzaliwa mara ya pili maana yake sio nini? Mtu awezaje kuzaliwa mara ya pili?"

Baada ya kumaliza kuandika, mmoja wenu asome kila barua kwa darasa zima. Kama itawezekana orodhesha wazo maalumu ubaoni. Mwambie mwanafunzi mmoja asome

Yohana 3:1-6 darasani. Waambie wayaangalie mawazo hayo mapya, mambo yo yote yale ya kufurahisha, au mawazo ambayo hayakufahamika. Jadilianeni mawazo hayo.

Sema, "Mawazo yako katika somo hili yamekuwa ya kufurahisha sana. Sasa hebu tuangalie Yohana 3:1-6.

"Nikodemu alikuwa Mfarisayo, mtawala katika Uyahudi. Kama walivyokuwa Mafarisayo alitii sheria za Musa. Mafarisayo walikuwa watu wenye kushika dini sana. Lakini Nikodemu hakuridhishwa na aina ile ya dini. Kulikuwepo na sheria nyingi, hivyo kuwa ilikuwa vigumu kabisa kutimiza sheria hizo zote. Alikuwa hana hakika kama sheria zote hizo zingemfikisha mbinguni.

"Nikodemu alikuwa amemwona Yesu akitenda mambo makubwa na alikuwa ameshawishika kuwa alikuwa mtu aliyetoka kwa Mungu. Alichotaka hasa kuelewa ni jinsi gani mtu aweza kuingia katika ufalme wa Mungu. Hakuuliza hilo swali kwa wazi lakini Yesu alielewa ni kitu gani alichotaka kuuliza. Kwa hivyo Yesu alimweleza yale yote aliyotaka kujua.

"Ni lazima azaliwe mara ya pili. Hii ni njia nyingine ya kusema kuwa ni lazima maisha yake yabadilike. Ni lazima awe mtu mpya. Ni lazima azaliwe na maji na kwa roho. Wakristo wanatofautiana kuhusu swala hili la maji kama ishara tu ya Neno la Mungu. (Waefeso 5:25-26; 1 Petro 1:23-25). Bado wengine wanayaona kama ishara ya Roho Mtakatifu (Yohana 7:37-39). Mambo haya yote ni muhimu katika kuzaliwa tena. Kutubu na kumpokea Kristo ni muhimu kwa kuzaliwa upya. Ubatizo hufuata hilo kwa wale ambao wamechagua kumtii Kristo.

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema, "Kama hujazaliwa mara ya pili, ina maana kuwa hujaingia katika ufalme wa Mungu bado. Kama ungekufa sasa hivi, ungekwenda jehanamu moja kwa moja. Kwa vyo vyote





"Hebu tujigawe katika makundi ya watu wanne au watano na tujadiliane pamoja maswali kadhaa. Kwa nini watu hugombana na kupigana wao wenyewe. Weka orodha ya majibu mbali mbali kwa lile swali la kwanza." (Wape dakika chache za kujadiliana.)

Sema: "Sasa soma Waefeso 4:25-32; 5:21. Mmoja asome kwa sauti. Ni mambo gani yaliyotajwa katika vifungu hivi yanayowafanya watu wasiweze kuhusiana? Je, tumeambiwa tufanye nini ili tuweze kuhusiana sisi wenyewe kwa upendo?"

**Maelezo**

Sema, "Jibu moja wazi lingewajia akilini mwenu mlivyokuwa mkisoma vifungu hivi vya Waefeso. Dhambi ndicho kitu kinacho wafanya watu wasiweze kuhusiana kwa upendo. Upendo ndicho kitu kinacho wafanya watu waweze kuishi pamoja kwa amani.

"Kifungu hicho kinatueleza ya kuwa tuziache dhambi za aina hiyo, hasa hasira. Kwa kuwa kanisa ni mwili, ni vizuri kama washiriki wake watajiamlia wao wenyewe. Paulo alifikiria akaona kuwa haingewezekana kuwaambia kuwa wanapaswa hata wasiwe na hasira. Labda wakati huo wengi walikuwa na tabia mbaya, lakini sasa ni lazima waheshimu haki za watu wengine.

"Hata ndivyo haitoshi kutokuwa na hasira peke yake. Ni lazima uuvae upendo. Kusamehe kunahitajiwa katika ushirika wa Kikristo. 'Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yako, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu' (Mathayo 6:14-15)."

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Kuna vitu viwili ambavyo vinaweza kutusaidia ili tuweze kuwa na uhusiano mzuri sisi kwa sisi.

3. *Je, unatofauti gani na wenye dhambi?* Yesu alizieleza njia za kawaida za mwenendo mwema kwa mfano kuwapenda wale wakupendao. Aliwatawanya kwa swali hili, "Je, hilo linafaida gani kwenu?" Mara nyingi watu wengi husema wao wanatenda haki na kuwa ni wema kwa jirani zao. Labda wako hivyo. Lakini swali sio "Mimi ni mzuri kiasi gani kuliko mtu wa kawaida?" Tusijilinganishe na jirani zetu. Tujilinganishe na Mungu.

4. *Mtakuwa wana wa yule mkuu aliye juu.* Kwa nini Wakristo wawe na utaratibu katika maisha yao? Utaratibu huu hutufanya sisi tuwe kama Mungu, kwani yeye ndivyo alivyo. Yeye huwa mpole kwa mtu amfurahishaye na tena kwa yule anayehuzunika moyoni mwake. Upendo wa Mungu huwakumbatia watakatifu wa wenye dhambi sawa sawa. Tunapaswa kuiga upendo wa jinsi hii.

5. *Jinsi unavyowatendea wengine nao ndivyo watakavyokutendea.* Kama unawahukumu wengine, ndivyo nao watakavyokutendea. Kama wewe ni mpole kwao, basi nao watakuwa wapole kwako. Kama unawapenda, hata wao watakupenda wewe. Jaribu jambo hili nawe utayaona matokeo yake.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Sema, "Mmoja wenu asome sehemu ya Utangulizi katika vitabu vyenu darasani." (Wape muda wa kusoma.) "Je, umeshapata shida kama hiyo katika maisha yako? Unaweza kuwa huna uhusiano mzuri na watu wengine, lakini bado utakuwa unawahitaji. Unaweza kuwa umegombana na kaka au dada yako nyumbani, lakini wakati huo huo unapenda kuwaona na kufurahia upendo wao. Wale wasio na kaka au dada, wangefurahi sana kama wengekuwa nao.





hupendi hali kama hiyo itokee kwako. Kuikwepa hali hii ni lazima uzaliwe mara ya pili; mpokee Kristo katika maisha yako tubu dhambi zako, na ubatizwe kwa jina la Yesu Kristo. Utapokea zawadi ya Roho Mtakatifu.

"Kama umeshazaliwa mara ya pili, soma ile sehemu ya "Mafunzo ya Sura Hii Kwangu" katika vitabu vyenu juu ya kichwa hiki na angalia tena ni nini unachotakiwa kufanya ili imani yako iwezekukua. Watoto wanatakiwa walishwe na kutunzwa kabla hawajakua. Angalia yale mambo ambayo unapaswa kufanya na ni yapi unayapuuza. Je; utaanza kuyatenda yote sasa?"

Wanafunzi warudie Kifungu cha Kukumbuka. Wakumbushe Kazi ya Kufanya katika vitabu vyao.

**Kuomba**

1. Waombee wokovu wale washiriki wa darasa lako ambao hawajazaliwa mara ya pili.

2. Omba kuwa wanafunzi watafurahi wakiona ya kuwa wengine wameokolewa.

3. Omba kuwa kanisa lako litatekeleza matakwa ya kuwaleta watu kwa Yesu, kuwabatiza na kuwafundisha Neno la Mungu (Mathayo 28:18-20).

SURA YA TATU

# MWILI WANGU

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Mwanzo 2:7; 3:19; Warumi 1:24-25; 3:13-15

Vifungu vya Leo: 1 Wakorintho 6:13-20

**Kifungu cha Kukumbuka:**

> "Basi ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu,ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana" (Warumi 12:1).

Kusudi la Somo Hili: Kuwasaidia wanafunzi wajifunze yale Biblia inayofundisha kuhusu mwili wa binadamu na jinsi ya kuutunza.

Vitu Vya Kusaidia Kufundisha: Karatasi na kalamu kwa kila mwanafunzi. Ubao au karatasi kubwa ya kuandika hicho kichwa.

**Msingi wa Somo Hili**

Mungu anaipenda miili yetu na jinsi tunavyoitumia. Mwanzo 2:7 inatueleza jinsi mwili wa mwanadamu ulivyoumbwa. Mungu alimuumba mwanadamu kutoka kwa mavumbi ya ardhi. Jambo hili la weza kuthibitishwa na Sayansi. Mwili wa mwanadamu umeumbwa na vitu vile vile ambavyo tunavipata ardhini pia.

Mwanzo 3:19 inatueleza matokeo ya dhambi katika mwili wa mwanadamu. Mwili wa mwanadamu unatakiwa ufanye kazi kwa nguvu, huwa unaugua,unazeeka, unakufa. Warumi 1:24-25; 3:13-15, vifungu hivyo vinatueleza watu hufanya nini na miili yao. Paulo ametaja matumizi mabaya ya ulimi, miguu na ashiki.



SURA YA KUMI NA MOJA

# MNAHUSIANAJE?

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Luka 6:27-38

Vifungu vya Leo: Waefeso 4:25-32; 5:21

**Kifungu cha Kukumbuka:**

> "Wapenzi, na tupendane; kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu, na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu" (1 Yohana 4:7).

Kusudi la Somo Hili: Kuwasaidia wanafunzi waelewe jinsi wanavyohusiana na wengine.

Vitu Vya Kusaidia Kufundisha: Ubao au karatasi kubwa. Andika hicho kichwa ubaoni.

**Msingi wa Somo Hili:**

Katika Luka 6:27-38. Yesu ametupa mawazo machache jinsi tuwezavyo kuutawala uhusiano wetu na wengine.

1. *Wapende adui zako.* Hapa Yesu anatufundisha kuwa tuiweke mioyo yetu mbali na chuki, hata kama unatendewa vibaya kiasi gani. Siyo hivyo tu, bali hata kuwatendea mazuri wale ambao wanataka kutuumiza sisi. Jambo hili ni kama haliwezekani lakini kwa msaada wa Mungu litawezekana. Tunaweza kuwapenda wale wanaotuchukia.

2. *Watendee wengine yale ambayo ungependa na wewe wakutendee pia.* Amri hii haisemi kuwa kuwatendea wengine kama wanavyotutendea sisi. Tuwatendee kama vile ambavyo tungependa wao watutendee. Tabia ya Mkristo haina nafasi ya kufanya mabaya. Ni lazima tujitahidi kutenda mambo mazuri.

**Kuomba**

1. Omba kuwa wanafunzi wako watapenda kuwatumikia wengine.

2. Omba kuwa wataelewa kwamba ufalme wa Mungu ni wa upendo, sio wa nguvu.

3. Omba kuwa wataelewa nini maana ya kuwa mtumishi.





Katika 1 Wakorintho 6:13-20 Paulo anakemea wale Wakristo, wanaofikiri kuwa uhuru wa Mkristo maana yake ni kufanya kitu cho chote unachotaka kufanya. Uhuru wa jinsi hiyo hutuongoza katika dhambi na matumizi mabaya ya miili yetu. Mji wa Korintho ulijaa watu waliokuwa malaya na makuhani wa kike. Wanawake waliwekwa katika mahekalu ya sanamu kwa madhumuni ya kumwabudu mungu wa kike aliyeitwa Venus. Uzinzi ulikuwa ni sehemu ya kuabudu kwenyewe.

Ujumbe wa Paulo kwa Wakorintho ulikuwa huu: Mwili wa Mkristo ni mali ya Mungu. Mungu ameununua kwa damu ya mwanawe. Kwa hivyo Wakristo lazima wamtukuze katika miili yao. Mwili wa Mkristo hauwezi kuwa wa malaya na wa Kristo wakati ule ule. Kwa hivyo Wakristo lazima waikimbie zinaa. Dhambi zingine zote hutendwa nje ya mwili lakini uzinzi ni dhambi inayotendwa ndani ya mwili.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Sema, "Leo tutajadiliana somo kuhusu mwili wa binadamu. Je, ni katika njia zipi ambazo watu huiharibu miili yao?" Baadhi ya majibu ni kwa kunywa pombe, kutumia dawa za kulevya, kuvuta sigara, kula kupita kiasi, kula vyakula vibaya, kutokuwa na mapumziko ya kutosha, kutofanya mazoezi ya mwili, kutouweka mwili katika hali ya usafi, na matumizi mabaya ya ashiki.

Sema, "Hapa kuna barua ambayo kijana mmoja alimwandikia mchungaji wake kuhusu somo hili la ashiki. Alihitaji msaada. Sasa anataka wewe ujifanye kama ndiye mchungaji. Ni lazima uijibu barua hiyo. Je, utamwandikia nini? Barua hiyo inasema hivi:

Ndugu yangu,

Tafadhali nisaidie. Nimefika mahali sasa nakata tamaa. Je, matakwa ya mwili si lazima yahudumiwe? Kwa nini Biblia inakataza mapenzi kabla ya ndoa? Kwa nini ni vibaya kuvitumia vile Mungu alivyoviumba? Nisaidie kama utaweza.

Wako akupendaye,
Aliyechanganyikiwa.

Mruhusu kila mmoja aandike barua fupi ya majibu.

Sema, "Sasa hebu tusome 1 Wakorintho 6:13-20 katika barua hiyo angalia yale mambo yatakayo kusaidia ili uweze kurekebisha barua yako ya majibu kwa kijana huyo.

**Maelezo**

Sema, "Jambo moja muhimu ambalo bila shaka umeligundua katika 1 Wakorintho 6:13-20 ni kuwa Mungu anajali sana miili yetu na jinsi tunavyoitumia. Kwa kweli miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu. Mungu hukaa ndani yake. Aliununua kwa thamani ya damu ya mwanawe.

"Katika kifungu hicho, tunaelezwa nini kuhusu matumizi mazuri ya miili? Tunapaswa kumtukuza Mungu kwa miili yetu. Hii maana yake ni kuwa ni lazima tuitumie kama vyombo vya haki. Ni lazima tuitumie kufanya mambo yale yanayo-mpendeza Mungu. Ni lazima tuwatumikie wengine, na kwa njia hiyo, tunamtumikia Mungu.

"Tusitumie miili yetu kama vyombo vya dhambi. Uzinzi ni kitu kimojawapo ambacho kinauharibu mwili wa binadamu. Kufanya mapenzi katika ndoa siyo kitu kibaya, lakini mambo ya mume na mke nje ya ndoa ni dhambi.

"Yesu alikuwa na mwili wa binadamu. Na nikwa kuutumia mwili huu aliweza kufanya kazi za Mungu hapa duniani. Hata baada ya kufufuka, bado alikuwa amevaa mwili huo huo, lakini kwa wakati huu ulikuwa umebadilika. Ulikuwa katika





mahali pa heshima. Walichukia kwa sababu Yakobo na Yohana waliuliza mapema, kabla wao hawajapata nafasi ya kufanya hivyo.

"Baadaye likaja fundisho. Unyenyekevu ndiyo tabia ya pekee inayowafaa wanafunzi wa Yesu. Nafasi hii siyo ya majivuno. Kila mwanafunzi wa Yesu ni lazima aache majivuno na awe tayari kuwatumikia wengine, ndivyo anavyo kuwa karibu zaidi na ufalme wa Mungu. Kusudi la Yesu kuja duniani lilikuwa kutumika. Utumishi huu unamwitaji kuwa ayatoe maisha yake kwa ajili ya wengine. Ni kwa njia ya kujitoa kama Yesu tu, hata mpaka mauti, ndipo maisha yetu yanaweza kuokolewa.

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Fundisho muhimu tunalojifunza katika somo hili ni kutumika. Dunia inahitaji watumishi sio mabwana. Mmoja wenu asome sehemu ya Utangulizi katika vitabu vyenu darasani.

"Kutumika maana yake ni kutimiza mahitaji ya watu wengine. Sasa hebu tusome sehemu ile ya Mafunzo ya Sura Hii Kwangu katika vitabu vyenu ili tuweze kujua ni mahitaji yapi twatakiwa tuyatimize. Ni hitaji lipi la muhimu sana? Je, inawezekana wewe kutimiza mahitaji ya kila mmoja? Hapana, hilo huwezi kulifanya. Lakini ni lazima tutimize mahitaji fulani. Ni lazima tujitahidi sana pale tulipo. Inakuwa vizuri zaidi wakati tunapowasaidia watu ili waweze kujisaidia wao wenyewe. Tusiwahimize kuwa wavivu. Soma Waefeso 4:28; 2 Wathesalonike 3:6-13.

"Kuna tofauti kati ya mahitaji na yale tunayotaka. Watu wanataka vitu vingi sana, lakini wanahitaji vitu vichache tu. Mtu mwerevu huhitaji vitu vichache sana lakini mpumbavu haridhiki na kitu cho chote. Tumeitwa ili tutumike na sio kutimiza yale watu wanayohitaji.

ya wanafunzi sita wa meza ile angechukuliwa ili agawe kile chakula. Kila mwanafunzi alipaswa apate kiasi kilicho sawa.

"Siku moja ilikuwa ni zamu ya Yakobo kugawa chakula. Baada ya kumaliza kukigawa kile chakula ilionekana wazi kuwa sahani yake ilikuwa na chakula kingi zaidi kuliko sahani zile zingine. Wale wanafunzi wenzake walianza kulalamika na Yakobo aliaibika sana. Hata aliondoka pale mezani bila kula."

Uliza, "Je, utamwita Yakobo mtumishi?" Wape muda kidogo kwa majadiliano. Sema: "Sasa hebu tuangalie Marko 10:35-45 na jaribuni kufuata yale yanayosemwa. Sote tuangalie tabia ya Yakobo na Yohana ilivyo katika hadithi hii. Pia tuangalie mafundisho muhimu ambayo twaweza kupata kutoka Marko 10:35-45."

**Maelezo**

Sema, "Yesu alikuwa amekwisha waeleza wanafunzi wake mara nyingi juu ya mateso ambayo angepata, lakini bado wanafunzi wake walikuwa wakifikiria kupata madaraka, ambayo walitegemea watayapata katika ufalme wa Yesu.

"Walipokuwa wakitembea njiani Yesu akawaambia tena kuhusu kuteswa kwake, na katika mazungumzo hayo Yakobo na Yohana wana wa Zebedayo wakamwendea. Walitaka wapate nafasi iliyo nzuri sana katika ufalme wake. Yesu aliwauliza kama walikuwa tayari kuteswa pamoja naye, lakini hata kabla hajawaambia hili, aliwaambia ya kuwa hawajui kile wakiombacho. Walikuwa wamesema wako tayari kukinywea kikombe cha Yesu. Yaani kikombe cha mateso. Basi Yesu akawaeleza ya kuwa hayo ni Mungu ayajuaye naye ndiye mwenye mamlaka ya kuwapa wale aliowawekea katika ufalme wake.

"Wale wanafunzi wengine walipoyasikia mazungumzo haya, walichukia sana kwa nini? Ni kwa sababu hata nao walitaka





hali tofauti na haukuwa tena chini ya mauti. Wakristo wataipita hali hiyo hiyo siku ya kufufuka. Miili yao itabadilika.

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema, "Biblia inatupa tahadhari nyingi kuhusu matumizi mabaya ya ashiki na hata miili yetu katika njia nyingine. Hebu tuangalie baadhi ya tahadhari hizi. Tayarisha wanafunzi tofauti wasome vifungu vifuatavyo; 1 Wakorintho 6:9-10; Wakolosai 3:5-6; 1 Wakorintho 5:11; 1 Wathesalonike 4:3-4; Waebrania 13:4.

"Sasa soma Mafunzo ya Sura Hii Kwangu katika vitabu vyenu kuhusu kichwa hiki." (Wape dakika chache za kusoma.)

Uliza, "Ni jambo gani katika kifungu hicho ambalo limekufurahisha sana? Je, kuna cho chote cha kusahihisha kuhusu mwili wako? Je, unafikiri mawazo ya yule Mkristo ambaye amealikwa katika sherehe ya ndoa au kifo na kadhalika ambako kuna pombe yawe nini? Je, kuna cho chote ambacho twaweza kufanya ili tuweze kuwasaidia watu wasiitumie miili yao kwa dawa za kulevya, sigara na vitu vingine ambavyo vinauharibu mwili wa binadamu? Waruhusu watoe maoni yao.

"*Ni wakati wa matendo.* Yesu alimwambia mtu mmoja, 'Nifuate.' Yule mtu akamwambia, 'Bwana nipe ruhusa kwanza niende kumzika baba yangu.' Lakini Yesu alimwambia, 'Acha wafu wawazike wafu wao, lakini wewe nenda na ukatangaze ufalme wa Mungu.' Mioyo yetu inapotutuma ni lazima twende mara moja."

Wanafunzi warudie Kifungu cha Kukumbuka mpaka wakielewe. Wakumbushe Kazi ya Kufanya katika vitabu vyao.

**Kuomba**

1. Omba kuwa wanafunzi watauona umuhimu alionao Mungu katika matumizi ya miili yao.

2. Omba kuwa wale ambao wamekuwa wakitumia vibaya miili yao, wataiona dhambi yao na kuikimbia.

3. Omba kuwa wao, pamoja nawe mtatambua njia za kumtumikia Mungu kwa miili yenu.





Yesu anayaona matendo haya ya huruma kama yametendwa kwake mwenyewe. Kuwatumikia wengine ni kumtumikia Mungu.

Angalia unyenyekevu wa watu hawa. Hawakufikiri ya kuwa yale waliyokuwa wanatenda kwa wenzao ni matendo mema. Kwao ni kitu cha kawaida kutenda mema siyo kitu cha kujivunia.

Je, mbuzi watakuwa nani? Hawa ni watu walio wachoyo, ambao hawayaangalii mahitaji ya watu wengine. Kwa matendo yao wanaonyesha ya kuwa wao ni kinyume cha Yesu mwenyewe, ingawaje wao wenyewe hawatambui hilo. Kwa hivyo wametengwa na furaha ya ufalme wake.

Je, umeanza kufikiri kuwa wokovu hupatikana kwa matendo mema? Hii siyo. Ni Mungu aliyeyabadilisha maisha ya wale waliowapenda wengine. Kutumikia ni matokeo ya mabadiliko hayo. Hawayafanyi hayo kwa nguvu zao wenyewe, bali kwa nguvu za Kristo.

Luka 17:7-10 inatufundisha kuhusu unyenyekevu. Tusijivunie mambo yale mazuri tufanyayo kwa jina la Kristo. Tunapokuwa tumefanya mazuri, tuna kuwa tumetimiza tu wajibu wetu.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Sema, "Kama mlivyoona ubaoni, kichwa chetu leo ni swali. Wewe u mtumishi? Hebu tuanze kwa kuangalia hadithi hii.

"Katika shule fulani ya sekondari, kijana mmoja alipewa wajibu wa kugawanya chakula katika chumba cha kulia chakula. Mtindo wa shule hiyo ulikuwa kwamba kila meza ingekuwa na bakuli ya chakula na bakuli ya supu. Mmoja kati

SURA YA KUMI

# WEWE U MTUMISHI?

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Mathayo 25:31-46; Luka 17:7-10

Vifungu vya Leo: Marko 10:35-45

**Kifungu cha Kukumbuka:**

> "Na mtu ye yote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu; kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi" (Mathayo 20:27-28).

Kusudi la Somo Hili: Niwasaidie wanafunzi wangu wajifunze kuwa kumtumikia mwanadamu ni kumtumikia Mungu.

Vitu Vya Kusaidia Kufundisha: Ubao au karatasi kubwa ya kuandika kichwa.

**Msingi wa Somo Hili**

Katika sura ya 24 na 25 ya kitabu cha Mathayo Yesu alifundisha kuhusu kuja kwake kwa mara ya pili pamoja na hukumu. Mafundisho hayo yanaishia na maelezo ya siku ya hukumu ambayo Mwana wa Adamu ataitoa duniani.

Watu wote wataitwa siku hiyo ya hukumu. Hukumu hiyo itahusu mambo yale ambayo sisi tumefanya. Wanadamu watagawanywa katika makundi mawili kama mkulima agawanyavyo mbuni na kondoo.

Je, kondoo ni akina nani? Hawa ni wale watu ambao waliwatumikia wenzao kwa vyakula, vinywaji, nguo na kushirikiana nao. Wao waliutesheleza mahitaji yao ya kimwili.



SURA YA NNE

# DUNIA YANGU

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Warumi 8:18-23; Ufunuo 4:11

Vifungu vya Leo: Mwanzo 1:26-31

**Kifungu cha Kukumbuka:**

> "maana Dunia ni mali ya Bwana na vyote viijazavyo" (1 Wakorintho 10:26).

Kusudi la Somo Hili: Kuwasaidia wanafunzi wauone wajibu wao kwa dunia (uumbaji wa Mungu).

Vitu Vya Kusaidia Kufundisha: Ubao au karatasi kubwa ya kuandikia kichwa cha somo hili.

**Msingi wa Somo Hili:**

Kuna uhusiano mkubwa kati ya mwanadamu na kuumbwa kwa ulimwengu. Mwanzo 1:26-31 inasema kuwa mwanadamu aliumbwa awe mfalme wa uumbaji. Mungu alimpa mamlaka juu ya vitu vyote. Dunia na vitu vyake vyote vyenye uhai vimewekwa chini ya utawala wa mwanadamu.

Uumbaji ulikusudiwa uwe wa manufaa kwa mwanadamu. Ulikuwa umpatie mwanadamu mahitaji yake pamoja na maendeleo yake yote. Kwa hivyo Mungu aliuumba ulimwengu wote uwe makao ya mwanadamu. Soma Mwanzo 1:29-30. Mwanadamu alipotenda dhambi; uumbaji nao ulihusika (Mwanzo 3:16-19). Dunia haikuwa na matunda ya kutosha. Mwanadamu alipaswa afanye kazi kwa nguvu ili aweze kupata chakula. Kuzaa kungekuwa kwa uchungu. Dunia ilianza kutoa magugu. Miili ya wanadamu nayo haikuandamana sana na roho. Hali ya uchovu, mateso na hata vifo viliingia.

Katika Warumi 8:19-22, Paulo anaeleza ya kuwa mwanadamu na hali ya asili vinahusiana kwani kwa ajili ya dhambi ya asili viumbe vyote pia viliungwa pamoja. Kwa hivyo wokovu wa mwanadamu utamaanisha pia wokovu wa viumbe vya asili. Viumbe vya asili vilihusika kwa ajili ya dhambi ya mwanadamu tunayoisoma katika Mwanzo 3:17: "...ardhi imelaaniwa kwa ajili yako..." Kwa hivyo katika Warumi 8, Paulo anaona viumbe vya asili vikingojea ukombozi kutoka dhambini na kuoza ambako kumeletwa duniani kwa ajili ya dhambi ya mwanadamu.

Mungu muumbaji anapenda viumbe vyote vitii. Anayo haki ya kuvishughulikia kwa njia yo yote apendayo. Viumbe vyote vyapaswa kutiishwa chini ya ubatili wake na vimpe utukufu na hekima.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Sema, "Leo tutaangalia kuumbwa kwa dunia yetu. Unaweza kukumbuka ya kuwa tulizungumzia juu ya uumbaji katika somo la kwanza, katika kitabu hiki, kuumbwa kwa mwanadamu na uhusiano wake na viumbe vingine Mungu alivyoumba. Leo tutaangalia kuumbwa kwa dunia na jinsi mwanadamu anavyoitumia."

Mmoja asome sehemu ya Utangulizi katika kitabu cha wanafunzi. Uliza, "Je, utayakubali majibu ya baba aliyomjibu binti yake? Je umeshakuwa katika hali ambayo uumbaji wa dunia umekusaidia kumjua muumba zaidi?

"Fikiria mabadiliko yote ambayo yametokea tangu Mungu aiumbe dunia hii. Je, unaweza kutaja baadhi yake?" Yaorodheshe haya ubaoni. Uliza, "Je, mabadiliko haya ni mazuri au mabaya? Sasa mchague mmoja asome Mwanzo





**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Kuna maswali matatu muhimu ambayo lazima kila mmoja wetu ajibu:

1. Je, umejenga maisha yako juu ya nini? Kama hunaye Kristo ndani yako, na kama huyatii kikamilifu mafundisho ya Kristo, basi umejenga nyumba yako juu ya mchanga. Unahitaji kujenga nyumba yako juu ya msingi imara, yaani Yesu Kristo.

2. Je, umeihesabu gharama ya kumfuata Kristo? Maisha ya Kikristo nayo pia yana matatizo, shida, njaa, majaribio na mateso. Watu wengine huamua kumfuata Kristo bila kujua kwa vitu kama hivyo vipo. Wanapovikuta hushangaa na kukata tamaa.

3. Je, unatumia vifaa gani katika kujenga? Je, vifaa hivyo vinaweza vikashinda majaribu yatakapo kuja?"

Wanafunzi warudie Kifungu cha Kukumbuka. Wakumbushe Kazi ya Kufanya katika vitabu vyao.

**Kuomba**

1. Omba kuwa wanafunzi wako wataelewa umuhimu wa kujenga maisha yao juu ya msingi wa haki.

2. Omba kuwa wataelewa kwa wazi gharama ya kuwa mwanafunzi na wawe tayari kulipa gharama hiyo.

3. Omba kuwa wataelewa wajibu wao katika kujenga maisha yako juu ya msingi huo na kuwa watasaidia wengine wafanye vivyo hivyo.

"Katika chombo hiki mnaona udongo wa mfinyanzi. Je, itakuwaje kama nikikuambia ujenge nyumba moja rahisi tu? Ungeweza kuifanya ikawa nzuri sana na ukajenga kwa aina yo yote. Je, hiyo ni nyumba ndogo ungeweza kuiita nyumba ya kudumu ambayo mtu aweza kuishi ndani yake? Maisha ya watu wengine ni kama mfano huo wa nyumba mara nyingi.

"Mmoja wenu asome sehemu ya Utangulizi katika vitabu vyenu kwetu sote. Kuna somo gani moja muhimu kuhusu maisha, ambalo umejifunza kutoka katika habari hiyo? Sasa soma 1 Wakorintho 3:5-15.

**Maelezo**

Sema: "Katika 1 Wakorintho 3:10-15, Paulo anatuambia mfano wa jengo kueleza hali ya kanisa na kazi ya kila mmoja aliye Mkristo. Kazi ya kila Mkristo ni kujenga juu ya msingi ule.

"Maisha ya Kikristo huanza pake mwamini anapompokea Kristo katika maisha yake. Hii ni kama kuweka msingi wa jengo. Kutoka hapo, Mkristo lazima akue. Kati ya mambo hayo kuna maombi, kujifunza Biblia, kuwashuhudia wengine kuhusu Kristo na yale aliyokutendea pamoja na kuhudhuria ibada na makutano mengine katika kanisa. Hii ni kama kujenga juu ya msingi.

"Kitu ambacho Paulo alikiona muhimu sana katika habari hii ni vile vitu tunavyo tumia katika kujenga msingi. Paulo anafananisha kazi ya wachungaji wa Kikristo na dhahabu na shaba (kifungu cha 12). Matendo kati ya haya ni yenye thamani yenye kudumu. Mengine hayafai na hayataweza kushinda majaribu. Dhahabu, fedha na mawe mengine yenye thamani yanaweza kupita katika moto bila kuharibiwa. Ila mbao, ukoka mkavu na mabua yatateketezwa na moto. Wakristo wengine hujenga maisha yao juu ya msingi wa Bwana Yesu Kristo. Hawa wanajenga na vifaa vile vyenye kudumu."





1:28. Uliza, "Je, kuna uhusiano gani katika kifungu hicho na mabadiliko ambayo tumeyataja hivi punde?"

Sema: "Tafadhali mmoja wenu asome Mwanzo 1:26-31. Mwingine tena asome Zaburi 8:3-6. Tutaandika uhusiano kati ya vifungu hivyo viwili ubaoni."

**Maelezo**

Sema: "Kuna mawazo matatu muhimu ambayo tunapata kutoka Mwanzo 1:26-31.

1. Mwanadamu ni taji ya uumbaji wa Mungu. Ni yeye pekee aliyeumbwa kwa sura ya Mungu. Hii inaonyesha tofauti kubwa iliyopo kati ya mwanadamu na wanyama wengine. Zaburi 8 inasema Mungu alimuumba mwanadamu mdogo punde kuliko Mungu. Amemwekea taji ya utukufu na heshima juu ya kichwa chake.

2. Mwanadamu alipewa mamlaka ya kutawala na kuiendeleza dunia. Hii ndiyo sababu tunapoiangalia dunia sasa hivi tunaona kuna mabadiliko. Mwanadamu anayatumia mamlaka aliyopewa na Mungu kuiendeleza dunia hii. Kwa sababu ya dhambi ya mwanadamu pia, tumeyaona mabadiliko mengi yasiyo mazuri.

3. Uumbaji ulikuwa ni kwa manufaa ya mwanadamu. Kusudi lake lilikuwa kumpa mwanadamu mahitaji yake pamoja na maendeleo yake yote. Hii haina maana kuwa sasa dunia ni mali ya mwanadamu kabisa. Katika 1 Wakorintho 10:26 tunasoma kuwa dunia na vyote vilivyomo ni mali ya Bwana. Hii maana yake ni kuwa mwanadamu yeye ni wakili tu wa mali ya Mungu. Dunia bado i chini ya utawala mkuu wa Mungu. Uumbaji wote lazima uupokee utukufu na heshima ya Mungu(Ufunuo 4:11).

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Mmoja wenu asome sehemu ya mafundisho ya sura hii kwangu darasani" Uliza, "Je, baadhi ya mawazo haya yalikuwa mapya kwako? Je, umeshapata kuyasikia?" (Wape muda wa majibu kama wanataka kuzungumza.) "Je tunaweza kujifunza nini kuhusu mawazo ya Ayubu katika vifungu hivyo vilivyokaririwa?

"Je unafikiri mawazo ya Mkristo yawe nini kuhusu Sayansi?" Wape muda wa majadiliano.

Sema, "Tumeona kuwa Mungu anao utawala mkuu na umilikaji wa ulimwengu alioumba. Tunapaswa kutumia uumbaji wake kwa kumwabudu. Tunapaswa kusaidia mabadiliko yaliyo mazuri na tuyakatae yale yaliyo mabaya.

Wanafunzi warudie Kifungu cha Kukumbuka mpaka waweze kukisema bila kusaidiwa. Wakumbushe Kazi ya Kufanya katika vitabu vyao.

**Kuomba**

1. Omba kuwa wanafunzi wako wataona ya kuwa dunia yenyewe sio mbaya. Kukosa katika kuitumia ndio kubaya.

2. Omba kuwa watatoa fedha zao, mali, muda na hata matumaini na vyote kwa Bwana, na watavitumia vyote kwa kumwabudu.

3. Muombe Mungu ajionyeshe kwako kwa njia ya uumbaji wake.





Kwa nini yule mjenzi mpumbavu hakufanya uamuzi wa busara? Alitaka atumie njia iliyo rahisi, ya kufurahisha na isiyo na usumbufu mwingi. Inaweza ikawa rahisi kwetu kuichukua njia yetu wenyewe kuliko ile ya Yesu, lakini mwisho wake ni maangamizi. Inaweza ikatuwia vigumu kuichukia njia ya Yesu, lakini ndiyo njia iliyo na usalama sasa na milele. Yule mjenzi mpumbavu vile vile hakufikiria vya kutosha. Hakufikiria mambo yajayo mbele. Aliyafikiria ya sasa tu. Mtu mwenye kufurahi ni yule aonaye mambo siyo katika mwanga wa muda fulani, lakini katika mwanga wa milele.

Katika Luka 14:28-30, Yesu alitumia mfano mwingine wa ujenzi ili kuonyesha ukweli mwingine wa tendo la kiroho. Ukweli huu ni juu ya kuhesabu gharama ya kumfuata Yesu. Mtu mmoja alianza kujenga lakini hakuweza kumaliza ule mnara aliokuwa anajenga. Alikuwa hana pesa za kutosha. Huu ni upumbavu. Alipaswa kuelewa tangu mwanzo ya kuwa angeweza kuumaliza huo mnara kwa vifaa vile alivyo kuwa navyo. Matokeo yake ni kuwa alipoteza muda wake pamoja na fedha. Watu walicheka upumbavu wake. Ni wajibu wa Mkristo kwanza kuhesabu gharama za kumfuata Yesu.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Sema: "Somo letu la leo ni juu ya kujenga maisha yetu juu ya msingi wa Yesu Kristo. Ni wangapi kati yenu wameshafanya kazi ya kujenga nyumba? Je, hiyo ilikuwa nyumba yako mwenyewe au nyumba ya mtu mwingine? Je, unaweza kutueleza hapo mwanzo mlifanya kitu gani? Je hiyo nyumba mpaka leo inatumika?

"Wengi wenu mmeona nyumba ambayo tunaiita nyumba ya kudumu. Kwa nini tunaziita nyumba za kudumu? Je, nyumba za jinsi hiyo zimejengwa namna gani?

SURA YA TISA

# UNAJENGA NINI?

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Mathayo 7:24-27; Luka 14:28-30

Vifungu vya Leo: 1 Wakorintho 3:5-15

**Kifungu cha Kukumbuka:**

> "Kwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa, mimi, kama mkuu wa wajenzi wenye hekima, naliuweka msingi, na mtu mwingine anajenga juu yake" (1 Wakorintho 3:10).

Kusudi la Somo Hili: Kuwasaidia wanafunzi waone wajibu tulionao sote katika kujenga juu ya msingi ambao Mungu ametuwekea katika maisha yetu.

Vitu Vya Kusaidia Kufundisha: Udongo wa mfinyanzi ulio na maji maji na ubao au karatasi kubwa.

**Msingi wa Somo Hili**

Yesu na waandishi wengine wa Agano Jipya walitumia mifano ya kujenga nyumba kufundisha mambo mengi ya kiroho. Mfano mmoja ni katika Mathayo 7:24-27. Watu wawili walipanga kujenga nyumba. Mmoja katika kutafuta mahali pa kujenga, alipata sehemu ya kuvutia katika mchanga na akajenga hapo. Upepo ulivuma na mvua iliponyesha, ile nyumba ilianguka kwa sababu haikuwa na msingi.

Mtu yule aliyekuwa na busara alitafuta mwamba, akajenga nyumba yake juu yake. Mvua iliponyesha na upepo ukavuma, ile nyumba ilisimama imara.

Mithali hii inatufundisha umuhimu wa msingi ulio bora katika maisha yetu. Msingi wa kweli pekee kwa maisha ni kuyatii mafundisho ya Yesu.



SURA YA TANO

# MUDA WANGU: WAKE AU WANGU

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Kutoka 20:8-11, Warumi 14:5-6

Vifungu vya Leo: Waefeso 5:15-20

**Kifungu cha Kukumbuka:**

> "Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo jambo lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu" (1 Wakorintho 10:31).

Kusudi la Somo Hili: Kuwasaidia wanafunzi waone kuwa muda wetu ni wa Mungu na kila wakati, ni zawadi kutoka kwa Mungu.

Vitu Vya Kusaidia Kufundisha: Chukua saa kama unazo. Labda unaweza kutumia picha zinazoonyesha saa na kuzishikanisha kwa karatasi kubwa, pia utahitaji ubao au karatasi.

**Msingi wa Somo Hili**

Mungu ndiye muumbaji na mwenye vitu vyote. Mwanadamu ni wakili tu wa mali ya Mungu. Yeye ni wakili wa mwili wake (1 Wakorintho 6:20) wa muda wake (Zaburi 90:12) na pesa zake (Luka 16:9-11). Kinachotakiwa kwa wakili ni aonekane kuwa mwaminifu. Siku moja kila mmoja atatoa hesabu ya uwakili wake.

Kutokana na mafundisho ya Agano la Kale, Mungu anahitaji sehemu moja ya saba ya muda wetu. "Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote..." (Kutoka 20:9-10).

Amri ya sabato ilikuwa ni pawe na siku ya mapumziko. Kwa Wakristo ina maana ya kutenga siku moja ya kutofanya kazi za kawaida. Hawatakiwi kuyatimiza matakwa ya ratiba ya shule au amri za mwajiri wao mpaka siku ya Jumatatu asubuhi. Tuko huru kuitumia siku hiyo kwa ibada na kujifurahisha.

Mungu alikusudia sheria hii rahisi iwe ni kwa manufaa ya mwanadamu na furaha yake. Ilimpa nafasi ya kupumzika kufanya kazi na kumwabudu Mungu. Lakini hata kufikia wakati wa Yesu Kristo, waalimu wa Kiyahudi walikuwa wameongeza mambo mengi katika amri hii, kuhusu yale mwanadamu hawezi kuyatenda siku ya sabato. Kwa hivyo siyo jambo la kushangaza kuwa tunapoisoma Injili, tunaona kuwa Yesu kila mara alikuwa na mabishano na viongozi hawa kuhusu amri hii hasa. Yesu alifundisha kuwa sabato ni kwa ajili ya mwanadamu, na siyo mwanadamu kwa ajili ya sabato. Vizuizi vya wanadamu pamoja na sheria, vilifanya sabato siku ya kuogopwa na ngumu.

Katika Warumi 14:1-12 Paulo anatoa maelekezo kuhusu wale walio dhaifu wa Imani. Tusiwadharau bali tuheshimu dhamiri zao. Tusiweke kishawishi kwa yule ndugu aliye dhaifu kwa kuonyesha uhuru wetu sisi wenyewe katika mambo ya kula, kunywa na siku maalum. Kila mtu athibitike katika akili zake mwenyewe maadamu sisi sote tumwadhimisha Bwana. Mtu mmoja afanya tofauti kati ya siku na siku; mwingine anaona siku zote kuwa sawasawa.

Kitu muhimu ni kukumbuka kuwa, Mkristo aangalie muda wake wote kama ni mali ya Mungu (Waefeso 5:15-20).

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Sema: "Leo tutaliangalia neno MUDA. Mmesha sikia watu wakisema kuhusu muda: Usipoteze muda wangu. Tafadhali





2. Kama kuna ye yote kati ya wanafunzi wako wanaopata majaribu au mateso, omba kuwa somo hili litawafariji.

**Ukweli Katika Maisha Yetu**

Sema: "Ebu tuangalie tena kifungu cha 5 na tuchunguze maneno haya yasemayo 'Mwanangu, usiyadharau marudia ya Bwana.' Neno 'usiyadharau' lina maana ya kuwa tutazame sababu ya kupata mateso, na siyo jinsi adhabu yenyewe ilivyotolewa.

"Kusudi la Mungu ni kuwa, tuwe na ushirika katika utukufu wake. Yeye atatumia hata njia zilizo mbaya ili afikie lengo lake. Wale Wakristo ambao wanashindwa kuuona ukweli huu, humlaumu Shetani kwa mateso yao. Shetani hawezi kuwatendea cho chote wana wa Mungu mpaka Mungu amruhusu yeye.

"Kitu muhimu kwa kila mmoja wetu ni kutambua yakuwa mateso ni makusudi ya Mungu katika kutuadhibu. Tunapaswa tutambue yakuwa mateso ni sehemu ya mapenzi ya Mungu na kwa makusudi yetu. Lakini lazima tuelewe ya kuwa kamwe siyo mapenzi ya Mungu sisi tuteseke kwa sababu ya kutotii kwetu au dhambi. Bwana wetu Yesu Kristo, kwa sababu ya huruma zake nyingi, anaweza kutumia mateso kama hayo ili kutufundisha. Lakini yeye hazifurahii dhambi zetu.

"Soma sehemu ya Mafunzo ya Sura Hii Kwangu kuhusu kichwa hiki. Andika adhabu mbali mbali za mwenendo mzuri ambazo Mkristo aweza kupata kutoka kwa Mungu. Anapaswa kukumbuka kuwa hii ni mifano michache tu. Kunayo mingine mingi."

Wanafunzi warudie Kifungu cha Kukumbuka. Wakumbushe Kazi ya Kufanya katika vitabu vyao.

**Kuomba**

1. Omba kuwa wanafunzi wako watakubali adhabu ya Mungu kama kitu cha kawaida cha maisha kwa Mkristo.





chunga muda. Fika muda ule ule. Usichelewe. Watu husema muda ni dhamana. Leo nataka tuangalie neno muda kama zawadi yetu kutoka kwa Mungu.

"Mmoja wetu atusomee sehemu ya Utangulizi." (Wape muda wa kusoma.) "Hadithi hii haina mengi kuhusu muda. Ni somo la kiwakili. Lakini mwanadamu ni wakili wa muda wa Mungu.

"Wengine wenu wanazo saa." (Onyesha picha zako za saa kama unazo.) "Je, ni nini muhimu wa kuwa na saa? Kwa nini watu wanatumia pesa nyingi kwa kununua saa?

"Hebu jifikirie wewe mwenyewe. Je muda una umuhimu gani kwako wewe? Je unapoteza muda wako, au unautumia vema? Tafadhali mmoja asome Waefeso 5:15-20 darasani. Wote tuangalie mawazo yaliyo muhimu katika habari hii. Labda tunaweza kujadiliana mawazo haya.

**Maelezo**

Sema, "Kuna mambo matatu ya ukweli yanayotokana na Waefeso 5:15-20.

1. *Muda ni zawadi kutoka kwa Mungu.* Kwa hivyo Mkristo **auone** muda wake wote kama ni mali ya Mungu. Asipoteze **wakati**. Hata hivyo hii maana yake si kuwa Mkristo afanye **kazi** wakati wote. Biblia inatufundisha kuwa lazima, pawepo **nafasi** ya kazi na kupumzika.

2. *Hakuna nafasi kwa maisha yasiyo na mpango wa mawazo.* Mkristo asiishi kama watu wengine, wasio na busara waishivyo. Ni lazima ajihadhari na kukataa vishawishi. Kifungu cha 18 kinataja dhambi ya ulevi. Jambo hili lilikuwa la kawaida kwa watu wasio Wakristo, na ni dhambi ambayo haiko peke yake. Mara nyingi imefuatwa na ujinga, Kutumia lugha mbovu, uasherati na mengine mengi.

3. *Tunapaswa kutumia muda wetu kwa kutenda mema.* Tusiwe wapumbavu bali tutumie muda wetu kuelewa na kuyatenda mapenzi ya Mungu. Tunazo karama za kiroho, akili na uwezo mwingine mwingi. Tuutumie kwa kuwatumikia wengine na kumtumikia Mungu.

**Ukweli Katika Maisha Yangu**

Sema: "Angalia ile sehemu ya Mafunzo ya Sura Hii Kwangu katika vitabu vyenu. Soma sehemu hiyo na orodhesha mambo manne yaliyotajwa hapo. Kila baada ya jambo moja andika yale utafanya ili uweze kuyatumia katika maisha yako." Wape muda wa kutosha kwa kazi hii.

Sema: "Labda wewe ni mmoja kati ya wale ambao hawajautumia muda wao kwa ukamilifu. Kwa hivyo umekuwa ukipoteza muda au "kuua" muda. Sasa umeelewa ya kuwa muda ni zawadi kutoka kwa Mungu. Unapaswa utubu dhambi yako ya kupoteza muda na kumwomba Mungu akusaidie kutoka sasa jinsi ya kutumia muda wako kama atakavyo kuongoza. Utatumia kila nafasi kutenda mema.

"Mwisho, ni lazima ujibidishe kuondoa uzembe, uvivu na uchelewaji. Unakumbuka ya kuwa mambo mengi ya Wakristo hayana nguvu sana kwani watu wengi huchelewa, na kwa hivyo yale yaliyopangwa kufanywa hufupishwa. Watu hao hao watafika katika sehemu zao za kazi wakati uliopangwa. Je, ni jambo lisilo hitaji nguvu kufika katika muda uliopangwa kwa ajili ya kumwabudu Mungu?

Wanafunzi warudie Kifungu cha Kukumbuka. Wakumbushe Kazi ya Kufanya katika vitabu vyao.

**Kuomba**

1. Ombea kuhusu jinsi wewe mwenyewe unavyotumia muda wako. Mwombe Mungu akuonyeshe kama unayo hatia kwa kupoteza muda.





wale watu waliokupa adhabu siku nyingi zilizopita? Je, unawapenda au unawachukia?

"Tafadhali mmoja wenu asome sehemu ya Utangulizi katika vitabu vyenu kwa darasa." Wape muda wa kusoma.

Uliza: "Ni kwa njia ipi unafikiri kuwa baba yake John alikuwa amefanya vema? Ni kwa njia zipi unafikiri angeweza kukosea? Mmoja wenu asome Waebrania 12:5-11 darasani."

**Maelezo**

Sema: "Habari tuliyosoma sasa hivi inatueleza kwa wazi kabisa kuwa Mungu kama Baba mwenye upendo hutumia majaribu na mateso ili kuwafundisha watoto wake na katika kuwafundisha mwenendo mzuri. Wale Wakristo wa kanisa la mwanzo, walipata kila aina ya majaribu na mateso. Wangeweza kukata tamaa. Hata wengine wangeweza kufikiri ya kuwa Mungu hawapendi. Mwandishi wa Waebrania anawaeleza ya kuwa wasikate tamaa kwa ajili ya mateso yao. Mungu anawatendea hayo kama wanawe.

"Mwandishi anatoa mfano wa kibinadamu. Hapa duniani tunaye baba wa kutufunza mwenendo mzuri. Wanafahamu ya kuwa watoto wakiwa hawana mwenendo mzuri, basi wataharibika. Baba hawaadhibu watoto wake kwa sababu hawapendi. Hufanya hivyo kwa sababu anawapenda wanawe. Ni lazima awafunze mwenendo mzuri.

"Bila shaka katika kufunza mwenendo mzuri lazima pawe na kuteseka. Hakuna anayependa jambo hili, lakini matunda yake ni ya thamani kubwa. Thamani yake ni sawa na mateso yenyewe. Kitu cha thamani ni kuwa '...matunda ya haki yenye amani' (Waebrania 12:11). Mungu anatutaka sisi tushiriki naye utakatifu wake."

Mungu pia alitunza afya zao pamoja na nguo zao. Ingawa walisafiri safari ya miguu katika nchi iliyokuwa jangwa kama hiyo, lakini hawakuwa na shida ya miguu yao kuvimba. Mungu aliwakinga na maumivu yote. Hili lilikuwa kusudi la kuwaonyesha yakuwa Mungu sio muumbaji tu. Yeye pia huifadhi. Walipaswa kumwamini Mungu mwema na mwenye nguvu kama hiyo.

Katika miaka hiyo yote ya kuelimishwa huko jangwani, Mungu aliwaweka watoto wake kuwa na mwenendo mzuri. "Nawe fikiri moyoni mwako, ya kuwa kama vile baba amrudivyo mwanawe, ndivyo Bwana, Mungu wako, akurudivyo" (Kumbukumbu la Torati 8:5). Baba huwarudia watoto wake kwa sababu anawapenda; naye Mungu hufanya hivyo kwa watu wake ambao anawapenda. Kwa muda wa miaka 40 Mungu alikuwa amewarudia na kuwalisha kwa mana. Nguo zao hazikuchakaa wala miguu yao haikuvimba. Vyote hivi vilikuwa ni kwa ajili ya kuwafundisha ili wamwamini Mungu na waishi kwa neno lake.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Sema, "Leo tutaangalia neno mwenendo mzuri. Mwenendo mzuri maana yake ni kuwa na tabia nzuri au matendo mazuri. Yaani ni kufundisha tabia. Ufundishaji huu unaweza kuwa wa aina nyingi. Lakini leo tutaangalia moja ya aina hizo. Aina hiyo tunaiita 'adhabu.' Tutaangalia kazi ya adhabu katika kufunza tabia.

"Karibu kila mmoja wenu hapa amekwisha pata adhabu. Adhabu ile labda ilitoka kwa mzazi wako, mwalimu wako, mkuu wa shule au kiranja wako wa shule. Je, ulijisikiaje katika adhabu hiyo? Je, ulijilaumu mwenyewe au ulimlaumu yule aliyekupa ile adhabu? Je, mawazo yako sasa ni nini kuhusu





2. Omba kuwa wanafunzi wako wataweza kujifunza umuhimu wa kutumia muda vema. Omba kua utajifunza umuhimu wa matumizi mazuri ya wakati wa mapumziko.

3. Omba kuwa mfano wako na ule wa wanafunzi wako utaenea kwa wengine katika kanisa lako ili watumie muda wao vema.

SURA YA SITA

# MAUMBILE YANGU: YAKE AU YANGU

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Mwanzo 1:26-27, Wagalatia 2:20

Vifungu vya Leo: Waefeso 4:22-24; Wagalatia 5:17-25

**Kifungu cha Kukumbuka:**

> "Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano huo huo toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho" (2 Wakorintho 3:18).

Kusudi la Somo Hili: Ni kuwasaidia wanafunzi wajifunze kuishi kwa mfano wa Mungu.

Vitu Vya Kusaidia Kufundisha: Ubao au karatasi kubwa. Kama utaweza, tengeneza vyungu vidogo (visivyo chomwa) na tena uchukue vijiti vidogo vilivyokauka.

**Msingi wa Somo Hili**

Mwanzo 1:26-27 inatueleza ya kuwa Mungu alimuumba mwanadamu kwa sura yake mwenyewe; jinsi yeye alivyo. Hii siyo sura ya kimwili. Mungu ni Roho. Naye hana mwili kama tulionao. Mwanadamu amevaa sura ya Mungu katika hali yake ya asili, katika matendo yake ya dhamiri, na katika mwenendo wake wa kuhusiana na viumbe wengine. Mungu alimpa mwanadamu uhuru wa kuamua.

Kwa vile tumeumbwa kwa mfano wa Mungu tunaweza kumfahamu yeye. Kwani kama hatukuumbwa kama Mungu,



SURA YA NANE

# MWENENDO MZURI

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: Kumbukumbu la Torati 8:2-5

Vifungu vya Leo: Waebrania 12:5-11

**Kifungu cha Kukumbuka:**

> "Basi kama mkiwa hamna kurudiwa, ambako ni fungu la wote, ndipo mmekuwa wana wa haramu ninyi, wala si wana wa halali" (Waebrania 12:8).

Kusudi la Somo Hili: Kuwasaidia wanafunzi waone kusudi, maana na matokeo ya matendo mazuri.

Vitu vya Kusaidia Kufundisha: Ubao au karatasi kubwa ambayo utaandika kichwa cha somo hili.

**Msingi wa Somo Hili**

Katika Kumbukumbu la Torati 8:2-5 Musa anawataka watu wa Israeli wakumbuke yale yaliyowatokea zamani, hasa jinsi Mungu alivyowatendea. Aliwakumbusha kuhusu hali yao ilivyokuwa kule Misri, safari yao mpaka kufika mlima wa Hori na kutoka hapo mpaka kwenye ukingo wa mto Jordani. Safari hii iliwachukua miaka 40 jangwani.

Kule kutangatanga jangwani ilikuwa ni adhabu, pia walitakiwa wawe watu wanyenyekevu. Mungu aliwapa chakula lakini kila mara hakikuwa kile chakula ambacho walikihitaji. Kiliwafanya waweze kuishi, lakini hakikuwafurahisha kwa ladha yake. Mungu aliwatendea hili ili awaonyeshe ya kuwa uhai wa kweli hautokani na vitu vya mwili tu, lakini kutoka katika Neno la Mungu. Yesu alikariri kifungu hiki hiki wakati alipojaribiwa kule jangwani.

**Ukweli Katika Maisha Yangu**

Sema, "Labda sasa unajisemea mwenyewe, 'Jambo hili linaonekana la ajabu, lakini nitalifanyaje?' Hapa kuna yale ambayo lazima ufanye. Ni lazima kumpokea Kristo kama Bwana wako. Hii ina maana gani? Ina maana kuwa yeye ni mtawala katika maisha yako. Tunapomkubali Kristo kama Bwana, tunampa ruhusa ya kututawala na kuwa Bwana wetu. Tunamtegemea atuongoze katika mambo yafuatayo katika maisha yetu: mwelekeo wetu, hisia, mahusiano, mawazo, tabia, matumaini, upendeleo na mengine mengi. Je, Kristo ataongozaje maisha yetu?

1. *Kwa njia ya Roho Mtakatifu.* Roho Mtakatifu hufanya mambo mengi katika maisha ya Wakristo. Moja wapo ni kule kutuongoza katika ukweli. Lingine ni kutuonyesha dhambi ni ipi (Yohana 16:18). Wakati tukiwa katika hatari ya kutenda dhambi au kuangukia dhambini, Roho Mtakatifu atatuambia. Yeye atatufanya wenye hatia mpaka tutubu dhambi zetu.

2. *Kwa njia ya Biblia.* 'Kila andiko, lenya pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema' (2 Timotheo 3:16-17).

3. "Hebu sasa sote tuangalie ile sehemu ya Mafunzo ya Sura Hii Kwangu katika vitabu vyenu ili tuweze kupata msaada zaidi kuhusu somo hili. Katika kuyaangalia hayo, ni katika njia zipi nyingine Kristo hutawala maisha yetu?

**Kuomba**

1. Omba kuwa wanafunzi wataelewa jinsi ya kufahamu mapenzi ya Mungu.

2. Omba kuwa watakapoyatambua mapenzi ya Mungu watakuwa tayari kuyatekeleza hata kama ni kwa gharama gani.





hatungeweza kumfahamu. Mhubiri 7:29 inasema kuwa Mungu alimuumba mwanadamu mwenye haki.

Mungu alipomuumba mwanadamu, alimuumba akiwa na dhamiri iliyo kamilifu. Vitu kama tamaa, uchoyo na chuki hapo mwanzo havikuwepo. Mawazo yake yalikuwa mema. Hisia zake zilikuwa njema na alifikiria kabla ya kutenda jambo. Uamuzi wake ulikuwa mzuri mpaka siku ile aliyotumia nguvu zake za kuchagua kwa kuchagua mabaya badala ya mema.

Hapa mwanzo Mungu na mwanadamu walikuwa marafiki wazuri. Waliongea na kutembea pamoja. Walitayarisha mipango mikubwa jinsi sayari hii yetu itakavyojazwa watu na jinsi itakavyoendelezwa.

Dunia ilitakiwa ionyeshe utukufu wa Mungu kwa ulimwengu wote. Mwanadamu alitakiwa awe ndiye rafiki wa karibu kabisa wa Mungu, mshiriki mwenzake katika kuilima na kuiendeleza dunia. Mungu hakutegemea kumlazimisha mwanadamu kumtii au kumpenda. Lakini tangu mwanzo alimwahidi zawadi ya mti wa uzima kama angemtii.

Hali aliyonayo mwanadamu sasa, siyo ile ya asili. Dhambi imeharibu sura ya Mungu katika mwanadamu. Dhambi imeharibu kila sehemu ya haiba yake - yaani mwili wake, akili yake, roho yake na hata moyo wake. Lakini kwa njia ya Kristo, sura ya Mungu inaweza kumrudia tena mwanadamu.

Hii inawezekana kwa kumpokea Kristo katika maisha yetu. Ili tusiwe ni sisi tena tunaoishi bali awe Kristo ndiye aishie ndani yetu. Soma Wagalatia 2:20.

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

**Utangulizi**

Sema, "Leo tutajifunza yale Biblia inayotuambia kuhusu maumbile yetu. Tumeshagusia baadhi ya mambo hayo.

Tumejifunza kuwa mwanadamu aliumbwa kwa sura ya Mungu. Yeye ni taji la uumbaji wa Mungu. Alipewa mamlaka ya kutawala na kuendeleza dunia. Hakuna viumbe wengine ulimwenguni ambao tunaweza kuwalinganisha na mwanadamu.

"Pia tunaelewa ya kuwa hali aliyonayo mwanadamu sasa hivi siyo ile hali yake ya asili. Dhambi imeharibu sura ya Mungu katika mwanadamu. Lakini sasa, kwa njia ya Kristo, ile sura ya Mungu inaweza kumrudia tena mwanadamu. Katika somo hili tutajifunza jinsi jambo hili litakavyotekelezwa.

"Hapa kuna vyungu vidogo vya udongo. Nakutaka wewe ukichukue kimoja na kuharibu sura yake yaani kukipasua, baadaye jaribu kuviweka hivyo vipande pamoja tena ili kuipata ile sura yake ya mwanzo. Jaribu sana uwezavyo kuviweka pamoja ili upate ile sura ya mwanzo. Pia chukua kijiti na kivunje. Kirudishe tena katika ile hali yake (kabla ya kuvunjwa)." Wape dakika chache.

Sema, "Mmefanya vizuri kwa kufuata masharti, lakini hamkuweza kuvirudisha vitu hivyo kikamilifu katika ile hali yake ya mwanzo. Kwa njia fulani vinaonekana tofauti. Sasa hebu tuangalie Waefeso 4:22-24 na Wagalatia 5:17-25. Je, ni mawazo gani katika vifungu hivi yaliyo sawa na yale uliyogundua katika kuvivunja vile vijiti au katika kuvipasua vyungu vile?"

**Maelezo**

Sema, "Vifungu hivi viwili vya habari vinatueleza jinsi tuwezavyo kuirudisha sura ya Mungu tena kwetu. Tumeamriwa kuuvua utu wa kale na kuuva utu upya. Tukitembea kiroho na siyo kutimiza mahitaji ya mwili. Hebu tuangalie kwa undani zaidi maneno haya mawili - utu wa kale na utu upya.





"Kabla sijawaambia kile ninachokifanya, hebu kwanza niwaulize swali. Ni mapenzi ya nani yaliwatawala sasa hivi? (Yakubali majibu yote.) Baadhi yenu wanasema ni mapenzi yenu wenyewe yaliyotawala vitendo vyenu. Wengine wanasema mapenzi yangu yaliwatawala ninyi. Haya, kama mimi nina nguvu kiasi hicho, hebu tujaribu tena. Hapa kuna mshumaa" (uwashe mshumaa kwa kiberiti) "sasa, kila mmoja aje na ajaribu kuweka kidole chake katika moto huu kwa dakika moja. Kwa nini hakuna hata mmoja anajitokeza?

"Jambo moja ni hili. Hamfanyi kila jambo ninalo waambia mfanye. Lazima pawepo na mapenzi ya watu wawili, yenu na yangu. Na mnaelewa kuwa tunafanya hivyo kwa Mungu. Wakati mwingine tunakataa kumtii, tukifikiria kuwa gharama ya kumtii ni kubwa sana. Tunaweza kumtii au kutomtii. Tunapaswa kuchagua kama tuyafanye mapenzi ya Mungu au mapenzi yetu sisi wenyewe. Sasa hebu tusome Mathayo 6:9-10; 7:21; Wakolosai 3:12-17." (Wachague wanafunzi kusoma.)

**Maelezo**

Sema: "Kiini cha mahubiri na mafundisho ya Yesu yalikuwa ni ufalme wa Mungu. Ufalme wa Mungu ni wakati mapenzi ya Mungu yanatendwa hapa duniani kama yalivyo huko mbinguni. Ili uwe na ufalme huo lazima uwe tayari kuyatenda mapenzi ya Mungu. Wale ambao hawamtii Kristo hawawezi kuwa wa ufalme wake (Mathayo 7:21). Yesu alitufundisha kuomba hivi: "...Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni' (Mathayo 6:9-10).

"Ni mapenzi ya Mungu kuwa tutauvua utu wetu wa kale na kuvaa utu upya. (Wakolosai 3:12-17). Vifungu hivi vinaeleza kuhusu vazi la utukufu. Sisi ni Yerusalemu mpya, na ni lazima tuishi kama Yerusalemu mpya. Umbo jipya ambalo tutakuwa nalo ni pamoja na huruma, usikivu, uvumilivu, subira, kusameheana na upendo. Hivi ni kwa wale wa ufalme wake.

Mungu. Mungu alimwagiza Sauli aende na kuwaangamiza Waamaleki. Hili lilikuwa ni jaribio la mwisho baada ya lile la kwanza la 1 Samweli 13 ambalo halikuleta toba. Kuangamizwa kwa Waamaleki, kwa ajili ya maovu yao kwa Waisraeli kulikuwa kumenenwa tangu zamani (Hesabu 24:20, Kumbukumbu la Torati 25:17-19).

Wakati Sauli alipokwenda kupigana na Waamaleki alitimiza sehemu tu ya amri ya Mungu. Aliwaangamiza Waamaleki; lakini alimwacha Agagi, mfalme wao, pamoja na wanyama wao. Mungu aliona tendo hili lisilo kamilishwa kama kutomtii. Samweli alimkemea yule mfalme kwa kutotii kwake na kutangaza kuwa ufalme wake umepewa mtu mwingine. Ufalme ule ulipewa Daudi.

Umuhimu wa utii unafundishwa katika Agano Jipya. Mungu huwapa Roho Mtakatifu wale wanaomtii (Matendo 5:32). Mitume wa Yesu walielewa umuhimu wa kutii. Walikuwa tayari kuteseka kutoka kutomtii Mungu. Utii kwa Mungu ulikuwa umuhimu kuliko utii kwa mamlaka ya wanadamu (Matendo 5:29).

Paulo alifurahi kujiita mtumwa wa Kristo. Mtumwa hawezi kutenda jingine zaidi ya kumtii Bwana wake. Sisi tu watumwa wa Kristo au watumwa wa dhambi. Wewe ni mtumwa wa yule unayemtii (Warumi 6:16).

## KULIFUNDISHA SOMO HILI

### Utangulizi

Sema, "Kila mmoja asimame juu! Weka mkono wako wa kushoto juu ya bega lako la kulia. Weka mkono wako wa kulia juu ya goti lako la kulia. Inua mguu wako wa kushoto juu (kutoka ardhini au sakafuni). Sasa jaribu kukimbia hatua tano. Sasa rudini katika viti vyenu.





"*Utu wa Kale*. Hii ni ile hali yetu ya ubinafsi. Mungu alipomuumba mwanadamu, alipa uwezo wa kupenda. Upendo huu unaweza kuwa katika Mungu, kwako binafsi au viumbe wengine. Upendo wa kujipenda zaidi kuliko Mungu na wanadamu wengine ni dhambi. Angalia Wagalatia 5:19-21. Hali hii ya ubinafsi iliyo ndani yetu ni lazima tuitoe kabla Mungu hajaturudishia tena sura yake.

"*Utu Upya*. Huu ni utu wa Mungu, tunda la Roho Mtakatifu. Tunapompokea Kristo kama Mwokozi na Bwana wetu, yeye huja na kuishi ndani yetu kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Ni Roho Mtakatifu anayezaa ndani yetu matendo kama yale ya Kristo ambayo tunayapata katika Wagalatia 5:22-23."

### Ukweli Katika Maisha Yetu

Sema, "Tumeamriwa tuuvue utu wetu wa kale na tuuvae utu upya; Je, katika hali halisi maana yake jambo hili ni nini? Kuuvua utu wa kale maana yake ni kuwa tunapaswa tuukatae ubinafsi wa aina yo yote. Amri kuu kupita zote Yesu alisema ni 'Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na roho yako yote, na kwa akili zako zote.' Ya pili ni 'Mpende jirani yako kama nafsi yako.' Angalia Mathayo 22:35-39. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kupita hizi. Upendo ni kinyume cha ubinafsi.

"Soma sehemu ya Mafunzo ya Sura Hii Kwangu katika vitabu vyenu na mtafute maana ya kuuvaa utu upya." (Dakika tano zinatosha kusoma jambo hilo.) "Ni lipi kati ya mambo yaliyo orodheshwa unalolitekeleza? Ni yapi ambayo utaanza kuyatekeleza?" (Usihitaji majibu, lakini waruhusu wanafunzi wayafikirie majibu yao.) "Sasa hebu tuangalie Wagalatia 5:22-23 tena. Je, mtu ataelewaje kuwa wewe umeuvua utu wa kale na kuuvaa utu upya?"

Wanafunzi warudie Kifungu cha Kukumbuka. Wakumbushe Kazi ya Kufanya katika vitabu vyao.

**Kuomba**

1. Omba kuwa wanafunzi wako wataona kuwa, kuwa Mkristo siyo mwisho wa mapigano ya kushinda dhambi, bali ndio mwanzo.

2. Omba kuwa utaliona tunda la Roho katika maisha yako.

3. Omba kuwa watalipenda tunda hilo katika maisha yao wao wenyewe na watamruhusu Roho Mtakatifu kuzaa hilo tunda.



SURA YA SABA

# MAPENZI YANGU: YAKE AU YANGU

## KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Somo Kutoka: I Samweli 15:1-29; Matendo 5:29; Warumi 6:16

Vifungu vya Leo: Mathayo 6:9-10; 7:21; Wakolosai 3:12-17

**Kifungu cha Kukumbuka:**

> "Yesu akamwambia, Chakula changu ndicho hiki, niyatende mapenzi yake aliyenipeleka, nikaimalize kazi yake" (Yohana 4:34).

Kusudi la Somo Hili: Niwasaidie wanafunzi waelewe jinsi ya kuchagua kati ya kutumikia na kutenda mapenzi ya Mungu.

Vitu Vya Kusaidia Kufundisha: Utahitaji mshumaa na kiberiti. Ubao au karatasi kubwa.

**Msingi wa Somo Hili**

Sauli alitawazwa kama mfalme wa Waisraeli na nabii Samweli ambaye pia alikuwa mwamuzi chini ya maelekezo ya Mungu. Kwa kiasi fulani Sauli alikuwa mfalme aliyefanikiwa. Aliwashinda maadui wa Waisraeli yaani Waamoni, Wafilisti, Wamoabu na Wamaleki. Hata hivyo Sauli alikuwa anakosa moja katika maisha yake. Hakuzitia maanani amri za Mungu. Alizitii alipopenda na aliacha kuzitii alipopenda.

Siku moja alitoa kafara ya kuchomwa, kazi ambayo kwa sheria ni makuhani tu waliifanya. Samweli alimwonya Sauli kuwa alikuwa katika hatari ya kupoteza ufalme wake kwa ajili ya kutozitii amri za Mungu.

Kitabu cha kwanza cha Samweli 15:1-29 kinatueleza mfano mwingine wa kutotii kwa Sauli hata kuyapoteza mapenzi ya